**Jinsi tunavyowafikiria watu wengine ni muhimu kwa Mungu**

**TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.**

Siku moja Yesu alipoulizwa kwa kujaribiwa na Mwanasheria Myahudi kuhusu amri ipi iliyo kuu kuliko zote, alijibu kuwa mpende Bwana Mungu wako kwa Moyo wako wote na kwa nguvu zako zote na kwa mawazo yako yote na jirani yako kama nafsi yako. Ili kufafanua alikuwa na maana gani kuhusu jirani, alielezea mfano wa Msamaria mwema . Unaweza kuikuta hii katika Luka sura ya 10 mistari ya 25 hadi 37.

Tutarejea tena sehemu hii ya mafunzo ya Yesu katika somo lijalo, lakini itabidi uwe ndiyo mwanzo wa somo hili halikadhalika kwa sababu tunapotumia upendo wa Wakristo katika uhusiano na watu wengine, hata wageni (kama msamaria mwema alivyofanya), maagizo aliyotoa Yesu kwetu sisi na Mitume yatakuwa rahisi kuyaelewa na kuyafuatilia.

Ni rahisi kuwa wazuri kwa tajiri na kwa wenye madaraka, lakini tu kawaonea na kuwadharau wanyonge, maskini au wasiojiweza. Yakobo, ndugu yake Yesu anasema kwamba “kuwaheshimu watu”na aghalabu anatuasa kuhusu mawazo haya. Yakobo sura ya 2 mstari wa 1 hadi 9, kuna mengi yakufikiria kuhusu maneno haya na yana umuhimu wa kipekee katika nchi na jamii, yenye mchanganyiko wa mataifa, makabila au rangi za watu.

Ukatili na ugomvi kutokana na ukorofi katika miaka ya hivi karibuni katika sehemu nyingi duniani ni matokeo yanayoelezea watu wengine kuwa ni duni, wasiowaaminifu au wasiostaarabika, vikionekana kama ni sehemu ya mawazo ya asili ya Mwanadamu.

Aidha Biblia inasema kinyume chake kwamba mawazo na tabia kama hizo hazina nafasi katika mioyo ya wale watakaokuwa Wanafunzi wa Yesu.

Paulo, mtume wa Yesu aliishi wakati utumwa ukikubalika kama sehemu ya Utawala wa Kirumi. Kuwa miongozo na maagizo mengi katika Waraka wa Paulo kuhusu mahusiano kati ya wale mabwana na watumwa ambao walikuwa Wanafunzi wa Yesu.

Angalia waraka huu kwa Makanisa yaliyoko Galatia sura ya 3 mistari ya 26 hadi 29. Hapa Paulo anasema waziwazi kwamba Wanafunzi wote wa Yesu wako sawa mbele ya macho ya Mungu. Hakuna tofauti kati ya mwanaume na mwanamke kati ya rangi ya ngozi au jamii atokayo mtu.

Tunapozungumza na watu tunaoishi nao au kufanya kazi pamoja, ni rahisi sana kutumia maneno yenye kuashiria vurumai na kutokuelewana ambayo yatawaumiza au kuwakatisha tamaa wengine, na Yakobo aliandika juu ya jambo hili pia angalia katika Waraka wake sura ya 3 mistari ya 5 hadi 11. Maneno magumu yazungumziwapo hayawezi kurejewa kama ilivyo tofauti kwetu sisi zote katika utu, mara nyingi wale wenye hasira za haraka wanapaswa kuwa waangalifu. Mungu kupitia Malaika wake anajua mambo tunayoyazungumza.

Matumizi ya hukumu yanakuwa na umuhimu kwetu inapokuwa kati ya mema na mabaya, au iliyo kweli na isiyo kweli lakini tunapoitumia hukumu hiyo hiyo kwa watu wengine tunatakiwa kuwa waanglifu zaidi. Yesu anatupa ushauri wa maana kuhusu jambo hili na umeandikwa katika Mathayo sura ya 7 mistari ya 1 haadi 5. Kutokana na maneno haya pengine inawezekana ukaamua kutokumuhukumu mtu mwingine lakini siyo rahisi kushikilia msimamo huu. Yesu anaunganisha maagizo yake kwa mfano mdogo. Ufunuo wa kuyaelewa maneno yake ni kutokana na maelezo kuhusu, “Kuangalia kibanzi katika jicho la ndugu yetu”! Jambo hili linazua lawama mara moja kwa watu wengine, na huku tukipuuzia mapungufu yetu mbele za Mungu.

Kuna wakati ambapo tunatakiwa kuwa waangalifu katika maamuzi yetu na Yesu anatoa mfano katika Mathayo sura ya 7 mistari ya 15 na 16. Ushauri huu bila shaka ulikuwa na maana katika miaka ya mwanzo ya Kanisa la Kikristo wakati ambapo

kulikuwa na walimu wengi wa uongo ambao hata walidiriki kujiita Kristo. Halikadhalika ni muhimu leo ambapo kuna Makanisa mengi na walimu.

Aidha kipimo muhimu ni " Mtawatambua kwa matunda yao" Wanayofanya wanaume na pengine hata wanawake katika maisha yao yanakuwa wazi kuliko yale wanayohubiri.

Baada ya Yesu kuwachagua Wanafunzi wake alianza kuwafundisha jinsi ya kufanya mambo ambayo yangempendeza Mungu, na mengi ya mambo ya haya yamo katika Injili ya Mathayo sura ya 5,6,7. Sasa hebu na tuangalie kwa pamoja katika sura ya 5, tusome kuanzia mstari wa 21. Yesu ananukuu kutoka katika sheria za Kiyahudi za Musa ambazo zinaanzia miaka ya nyuma wakati Taifa la Israeli lilipo okolewa kutoka katika utumwa wa nchi ya Misri
Hapa anaeleza kwamba wakati wa Sheria za zamani zilithibiti matendo ya Wayahudi, sheria zake mpya zitakuwa mbele zaidi kwa kuthibiti mawazo yao na hata hisia zao. Anazungumzia juu ya hasira, maneno ya matusi na mawazo ya tamaa mbaya. Anazungumzia juu ya uvunjifu wa ndoa unatokea mara nyingi kutokana na tamaa ya uzinzi na wengine nje ya ndoa.

Katika mstari wa 33 Yesu ameonya juu ya kuapa kusikokuwa kwa ishara. Kwa kufanya hivyo wanatumia maneno ambayo wenzao watayakubali kuwa ni ya kweli na yakuaminika. Kwa bahati mbaya, wanachagua kutumia maneno ambayo ni Matakatifu kwa Mungu na ambayo amekataza kuyatumia. Hata kama tunafikiria tu katika mawazo yetu, ni muhimu kuwa daima tunakumbuka agizo lake katika Kutoka sura ya 20 msatri wa 7. Kama ulivyo utaratibu wa kawaida, Yesu anasema "Usiape kabisa – Mathayo sura ya 5 mstari wa 34. Ni afadhali kabisa kutokutumia viapo wakati wowote na hii inajumuisha Mahakama ya Sheria ikiwa tutajikuta katika mahali kama hapo. Aidha mara nyingi nafasi imewekwa kwa wafuasi wa Yesu kuthibitisha kabla ya kutoa ushahidi. Matumizi ya kuapishw kama njia ya kuelezea tufikirie nini juu ya wengine yamekwisha kushughulikiwa na Yesu katika maagizo yake kwamba tuwe waangalifu kwa yale tunayosema, mstari wa 22.

Katika mstaari wa 44, agizo la kuwapenda jirani zetu, hatua nyingi zaidi zimechukuliwa. Sasa Yesu anatuambia tuwapende maadui zetu! Kuwabariki wale wanaotulaani na kuwatendea mema wale wanaotuchukia! Kuwaombea hata wale watu wanaotudhuru. Haitakuwa rahisi kuyazingatia maagizo haya kwa kuwa hisia zetu za asili ni kufanya yaliyo kinyume. Hata hivyo ni wazi kuwa yote hii ni mifano tu iliyotolewa na Yesu jinsi tunavyowafikiria wengine na jambo hili ni la muhimu kwa Mungu.

Pengine msaada muhimu wa kutuongoza ni kuona jinsi Yesu alivyoonyesha kwa matendo kwa wale katili waliompiga na kumpigilia misumari katika msalaba. Maneno yake yaliandikwa na Luka katika sura ya 23 mistari ya 33 na 34. Ikiwa Yesu aliweza kusamehe akiwa katika maumivu na uchungu yumkini sisi tunaotaka kuwa Wanafunzi wake ni lazima tujifunze kufuata mfano wake ambao ni wa muhimu sana kwetu .

Majivuno na kiburi havina nafasi mbele ya Mungu, katika matendo yetu lakini muhimu zaidi ni katika mioyo yetu na mawazo.

Kwa kumalizia somo hili, hebu na tuangalie pamoja katika baadhi ya maneno ya Isaya sura ya 66 katika utabiri wake, mistari yaa 1 na 2. Inatupatia fununu ya mambo ambayo Mungu anataka kutoka kwetu na mwenendo wa utu wa kumpendeza Mungu.

**CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom**
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)